

ARIPO: KUSAWAZISHA ULINZI WA AINA ZA MIMEA BARANI AFRIKA

Kwa kipindi cha miaka michache iliyopita, Sekretarieti na nchi wanachama 10 wa Shirika la Kanda la Afrika Linalosimamia Hati Miliki za Kitaaluma (ARIPO) wamekuwa wakitayarisha sheria moja iliyosawazishwa ijulikanayo kama **Itifaki ya Kulinda Aina za Mimea (PVP)**. Itifaki hii inatokana na Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina za Mbegu (UPOV) wa mwaka 1991* na uliridhiwa katika jiji la Arusha, Tanzania, mnamo Julai 2015.


Itifaki ya ARIPO kuhusu Kulinda Aina za Mimea:

- ◆ inaanza katika kanda mfumo wa Kulinda Aina za Mimea ambao sio tu unapendelea wazalishaji wakubwa wa mbegu lakini pia hudhoofisha haki za wakulima wadogo kuwa huru kutumia, kubadilishana na kuuza mbegu ambazo zimehifadhiwa kutoka mashambani za aina inayolindwa;
- ◆ inawapa mamlaka Ofisi ya Shirika la ARIPO kuwapatia wakulima wakubwa wa mbegu Haki za Wazalishaji wa Mbegu zilizo na nguvu sana;
- ◆ inazifanya Haki za Wazalishaji wa Mbegu zilizotolewa na Ofisi ya Shirika la ARIPO kutambulika katika nchi zote wanachama wa Shirika la ARIPO;
- ◆ inarahisishia makampuni ya mbegu ya kigeni kunyakua mifumo ya mbegu katika bara la Afrika na kutumia kinyume na sheria aina za mimea inayopatikana kienyeji; na
- ◆ inabadilisha sheria na mifumo ya taifa ya Haki za Wazalishaji wa Mbegu.

Itifaki hii inapora mamlaka ya serikali kulinda haki za wakulima kuhusiana na matumizi ya aina za mbegu zinazolindwa.

Haitambui mifumo anuwai ya mbegu za wakulima wadogo, wala umuhimu wa uhuru wa mbegu za wenyeji.

Mchakato wa kutayarisha Itifaki hii haukuwa wa uaminifu au uwazi, na uliwatenga



wakulima, wakati wakijumuisha makampuni ya mbegu na makampuni mengineyo ya kigeni.

Ili kulinda haki za wakulima wetu, lazima tuhakikishe kwamba nchi wanachama wa Shirika la ARIPO **HAWAIDHINISHI** (hawaridhii) Itifaki hii na kuwa Mshirika Aliyeridhia Mkataba wa Itifaki. Iwapo haya yatatokea, Itifaki itawafunga wakulima wetu kisheria.

* UPOV 91 ni Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina za Mimea uliyotayarishwa na wazalishaji wa mimea kutoka Ulaya kwa ajili ya mifumo ya kilimo iliyo na matumizi makubwa ya viwanda.

